

**UZINDUZI WA KAMATI YA KAMATI YA BARAZA LA MAPINDUZI YA KUSHAURI  
NJIA ZA KUIJENGA UPYA KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA  
KIMUUNDO NA KIUTENDAJI ILI ITEKELEZE MAJUKUMU YAKE KWA UFANISI  
NA KULETA TIJA ZANZIBAR. TAREHE 22/4/2022**

Waziri Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman amefanya uzinduzi wa Kamati ya Baraza la Mapinduzi iliyopewa jukumu la kushauri njia bora za kuijenga upya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Kimuundo na Kiutendaji ili itekeleze majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Uzinduzi huo ulifanyika katika ukumbi wa Wizara ya Katiba Sheria, Utumishi na Utawala Bora Mazizini Zanzibar.

Katika Uzinduzi huo Mheshimiwa Waziri waliwataka wajumbe wa kamati hiyo kufanyakazi kwa bidii na uadilifu ili lengo la Viongozi wakuu wa Serikali liweze kufanikiwa.

Kwa upande wao wajumbe wa Kamati hiyo waliishukuru Serikali kwa kuwateua na wakaahidi kulitekeleza jukumu hilo kwa uwezo wao wote.

Wajumbe wa Kamati hiyo ni Mwenyekiti Profesa Hamed R. H. Hikimany na wajumbe ni Profesa Mohammed Hafidh Khalfan - Mjumbe, Bwa Juma Amour Mohammed – Mjumbe, bwana Abdalla Ussi Hamad - Mjumbe, Bi Huda Ahmed Yussuf – Mjumbe na Sheik Abdulla Talib Abdulla – Katibu wa Kamati

Wajumbe wa Kamati wakiwa katika picha ya pamoja na Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu – (O. R) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

